WHITE LAKE HIGH SCHOOL
P.O. Box 75787, Changanyikeni, Dar es Salaam, Tanzania.
Regn. No: S.1388
Tel: 0738 -783331 / 0738 -783332 / 0738 -783333
website: www.whitelakehighschool.co.tz / email: info@whitelakehighschool.co.tz

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WHITE LAKE

## Kwa Elimu ya Sekondari, Ngazi ya juu (Kidato Cha V na VI)

### 1.1. UTANGULIZI:

Hongera!

Kwa niaba ya Uongozi wa Shule ya Sekondari White Lake, tuna furaha kubwa kukujulisha kwamba mwanao……………………………………… ambaye alifanya mtihani wa usaili wa kujiunga na Shule ya Sekondari White Lake tarehe 01 mwezi 07 mwaka 2024 amefanya vizuri kwa kupata wastani wa daraja la ……… – NECTA 2023 kufuatia ufaulu huu, amepata nafasi ya kujiunga na kidato cha tano. Katika shule yetu kwa mwaka wa masomo mchepuo wa ……………… Karibu sana!

### 1.2. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo Mtaa wa Changanyikeni, Kaskazini mwa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kilomita 2.5 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam katika wilaya ya Kinondoni, Dar -es-Salaam. Ni Shule ya mchanganyiko kwa wanafunzi wa bweni tu. Maelezo zaidi kuhusu shule hii yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya shule: www.whitelakehighschool.co.tz

### 1.3. MASHARTI YA KUJIUNGA:

a) Fomu hii ya maombi ijazwe na kusainiwa na mwombaji na kurudishwa shuleni ndani ya muda uliowekwa / uliopangwa;
b) Udahili wa mwanafunzi utafanywa ofisi ya utawala White Lake Sekondari baada ya taratibu za usajili zinazostahili kukamilika;
c) Ada ya maombi (Joining Instruction) ya sh 20,000/= lazima ilipwe kwa akaunti Na. 22210006313 katika Benki ya NMB, gharama hizi hazirudishwi;
d) Ada zinaweza kubadilika wakati wowote kadri Bodi ya Shule itakavyoamua kulingana na mahitaji ya shule.
e) Shule inaweza kubadilisha masharti ya udahili/usajili wakati wowote itakapohitajika;
f) Mwanafunzi aliyedahiliwa anawajibika kwa usalama na matumizi salama ya mali binafsi na mali za shule;
g) Wanafunzi lazima wahudhurie darasani kila siku na kufikia kiwango cha mahudhurio kisichopungua 96%; vinginevyo hataruhusiwa kufanya mitihani;
h) Mwanafunzi LAZIMA apate wastani wa 70 kwa kila somo ili kuweza kuendelea na darasa linalofuata; vinginevyo atatakiwa kukariri darasa au kuhama shule;

## 1.4. Ratiba ya Shule na Mtaala:

**a) Mwaka wa masomo una mihula miwili:**

**(i) Julai hadi Disemba (Muhula l)**
- Mapumziko ya nusu muhula (wiki 2) mwezi Septemba
- Likizo ya mwezi mmoja (mwezi Disemba)

**(ii) Januari hadi Juni (Muhula wa II)** ○ Mapumziko ya nusu muhula (wikj 2) mwezi Machi / Aprili ○ Likizo ya mwezi mmoja (mwezi Juni).

b) **Ratiba ya kila siku (Saa za Darasani):**

(í) 01:30 asubuhi hadi 10:40 Jioni (Jumatatu hadi Ijumaa)

(ii) 03:00 asubuhi hadi 06:00 Mchana (Jumamosi) na Jumapili baada ya ibada. c)

**Mtaala:**

Mtaala unaotumika unazingatia mtaala wa elimu wa shule za sekondari nchini Tanzania.

**1.5. Ada ya Shule na malipo mengine:**

(i) Maelekezo ya Ulipaji wa Ada:

Muundo wa ada ya Shule ya Sekondari White Lake ni wa ushindani na wa bei nafuu. Ada ya shule hulipwa kupitia akaunti ya benki Na. **22210006313/22210006312** katika benki ya NMB. Malipo hayo hulipwa kwa mchanagnuo ufuatao: -

## KWA WANAFUNZI WA BWENI TU

| KATEGORIA | MUHULA I | MUHULA II | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Ada ya Shule | 1,500,000.00 | 1,000,000.00 | 2,500,000.00 |
| Chakula na Malazi | 1,100,000.00 | 880,000.00 | 1,980,000.00 |
| Michango mingine | 520,000.00 | 0.00 | 520,000.00 |
| **JUMLA** | **3,120,000.00** | **1,880,000.00** | **5,000,000.00** |

**TANBIHI:**

Kiasi cha kuanzia laki tatu (**Shs. 300,000.00**) kinapaswa kulipwa kushikia nafasi (ADVANSI), kiasi hiki kilipwe ndani ya siku tano baada ya mwanafunzi kufaulu mtihani wa usaili. Kwa yeyote atakayeshindwa kulipa kiasi hiki ndani ya muda uliowekwa, basi nafasi yake itaondolewa (Malipo haya ni sehemu ya ada). Ilipwe **kwenye Akaunti Na. 22210006313 Benki ya NMB** na risiti halisi ya malipo iwasilishwe shuleni Ofisi ya Uhasibu ndani ya siku hizo tano. Baada ya hapo uonane na ofisi ya taaluma kwa ajili ya usajili, na maelekezo ya kukamilisha usajili.

**(iii) Mahitaji yanayopatikana Shuleni baada ya kulipa Ada:**

a) Sare za shule (Suruali 2 kwa wavulana au sketi 2 kwa wasichana, mashati 2 meupe yenye lebo ya shule, sweta 1, suti 1, tai ya shingoni na gauni 2 za kushindia)
b) Gharama ya usafiri kwenda hospitali ikitokea changamoto ya kiafya. (Mzazi hakikisha mtoto ana Bima ya afya)
c) Kitambulisho cha mwanafunzi (ikiwa mwanafunzi atapoteza atalazimika kulipia)
d) Mfumo wa ShuteSoft (NMB)
e) Mzazi lazima aje na cheti kilichothibitishwa na daktari wa mwanafunzi mwenye tatizo Ia kiafya au kutokula baadhi ya vyakula. Mzazi atawajibika kulipa Shs **400,000.00** kwa muhula kwa huduma ya mlo maalum **(Special Diet)** ilipwe kwa taslimu.
f) Huduma ya kunyoa
g) Vifaa vifuatavyo: TRANKA, SAHANI, KIKOMBE, KIJIKO, MTO, SHUKA, GODORO, CHANDARUA na CHUPA YA MAJI, atapatiwa shuleni.
h) Mwanafunzi aje na begi la kubebea nguo tu likiwa na ukubwa wa kati.
i) Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule aliyokua anasoma atakazozitumia wakati anatayarishiwa sare za shule ya White Lake High School.

## 1.6. Mahitaji maalum ya mwanafunzi:

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:

**(A) Vifaa vya Kitaaluma:**

- Begi jeusi la shule;
- Faili la kutunzia mitihani;
- Saa ya mkononi;
- Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza;
- Madaftari 12 ya mazoezi (Counter books Quire 3) yanapatikana shuleni kwa pesa taslimu tsh 3,500/=kwa kila daftari moja. Madaftari yana nembo ya shule pamoja na picha mbalimbali za mazingira ya shule;
- Ream ya karatasi ya nakala yenye ukubwa wa A4100g/m; o Grafu 1 (Bunda moja);
- Vitabu vyote vya kiada vilivyopendekezwa kwa darasa husika.
- Rula, penseli, kalamu za wino (mweusi au bluu) za kutosha.

**(B) Sare za Shule:**

**(i) Sare za wasichana**

- Sketi 2 kijani ya jeshi (dark green) (**watapatiwa shuleni**);
- Mashati meupe 2 ya mikono mirefu na lebo ya shule (**atapatiwa shuleni**); o Jozi 4 za soksi ndefu nyeupe zinazofika chini ya magoti;
- Jozi 2 za viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba (**Vyenye kufunika mguu vyema**), viatu vyenye uwazi haviruhusiwi shuleni;
- Tai l (**atapatiwa shuleni**);
- T-shirt 2 za Shule (**atapatiwa shuleni**);
- Jozi 2 za nguo za kulalia (**Night dress**);
- Sanduku 1 la chuma (**atapatiwa shuleni);**
- Jozi 2 za jezi za michezo (**Aina ya jezi kulingana na darasa husika**); tafadhali wasiliana na uongozi kufahamu aina ya jezi inayohitajika; ni za kununua.
- Raba nyeupe za mazoezi (**zisiwe na rangi nyingine yoyote**);
- Chupa ya maji ya kunywa ( **atapatiwa shuleni**),
- Kufuli kwa ajili ya usalama wa vifaa vyake, ni la kununua.

**(ü) Sare za shule kwa wavulana:**

- Suruali 2 kijani ya jeshi (dark green) (**atapatiwa shuleni**);
- Mashati 2 meupe ya mikono mirefu na lebo ya shule (**atapatiwa shuleni**);
- Jozi 4 za soksi nyeupe ndefu kiasi;
- Jozi 2 za jezi za michezo (Aina ya jezi kulingana na darasa husika); tafadhali wasiliana na uongozi kufahamu aina ya jezi inayohitajika; ni za kununua.
- Suruali 2 nyeusi za kitambaa (upana wa chini uwe ni inchi 16);
- Raba nyeupe za mazoezi (zisiwe na rangi nyingine yoyote);

- Jozi 2 za viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba (vyenye kufunika mguu vyema);
- Mkanda mweusi wa ngozi wenye upana wa nchi 1.5");
- Tai l (**atapatiwa shuleni**);
- T-shirt 2 za shule (**atapatiwa shuleni**);
- Jozi 3 za pajama (night dress); aje nazo.
- Sanduku 1 la chuma ; (**atapatiwa shuleni**);
- Kufuli kwa ajili ya usalama wa vifaa vyakela ni la kununua.

**TANBIHI:** Hairuhusiwi kushona sare zinazopatikana shuleni nje ya shule ili kuepuka mkanganyiko wa vipimo na sare (rangi) zinazohitajika. Pia vifaa vyote vinavyopatikana shuleni visinunuliwe nje ya shule kuepuka usumbufu.

**(c) Mahitaji ya Bwenini:**

- Godoro la futi 2.5 x 6 pamoja na kava lake (**atapatiwa shuleni**);
- Mto na foronya 2 za kulalia. Rangi ya bluu kwa wavulana na rangi ya waridi (pink) kwa wasichana (**watapatiwa shuleni**);
- Chandarua 1 cha mraba chenye ukubwa wa futi 3 kwa 6 (**atapatiwa shuleni**);
- Mashuka 2 ya vitanda futi 4 kwa futi 6 rangi ya bluu kwa wavulana na rangi ya waridi (Pink) kwa wasichana (**atapatiwa shuleni**);
- Sabuni ya kuogea angalau pisi 12; aje nazo.
- Sabuni ya unga ya kufulia kiasi cha kutosha;
- Nguo za ndani za kutosha;
- Dawa 4 za meno na miswaki ya kutosha;
- Ndoo 1 yenye ujazo wa lita kumi kwa ajili ya kufulia;
- Mafuta ya ngozì au Losheni;
- Biblia (kwa Wakristo) na (Quran kwa Waislamu);
- Mwanafunzi anaporipoti, alete mojawapo ya vifaa vifuatavyo vya kufanyia usafi wa mazingira;
  - i. Ufagio mmoja (soft broom au hard broom);
  - ii. Mopa moja ya kudekia (Mopa na ndoo yake);
  - iii. Mopa moja ya kukaushia maji (rubber squeezer);
  - iv. Ndoo maalumu ya kuhifadhia taka (Dustbin);
  - v. Brashi maalumu za kusafishia kuta na vyoo, (moja tu kwa kila mwanafunzi);
- Pesa ya matumizi binafsi ya mwanafunzi iwekwe kwenye Ofisi ya Mhasibu pindi mwanafunzi anapowasili shuleni. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na au kuhifadhi pesa bwenini, na ikibainika adhabu kali itatolewa kwa mwanafunzi huyo; na ikiwa mwanafunzi atapoteza pesa bwenini, uongozi wa shule hautashughulika kwa namna yoyote.

# 2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

## 2.1. USULI / UTANGULIZI:

Bodi ya Shule ya Sekondari White Lake katika mkutano wake wa 4 uliofanyika tarehe 14 Julai 2018; ilipitia Kanuni za Shule ambazo zimekuwa zikitumika kuzifanyia maboresho ili kukidhi mahitaji. Sheria zilizopitiwa zimeanza kutumika tangu tarehe 15 Julai, 2018. Kwa hiyo, kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia.

## 2.2, Madhumuni ya Sheria za Shule

Sheria za Shule ya Sekondari White Lake zinalenga:-

a) Kukuza tabia njema, nidhamu na heshima shulení;
b) Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanamaliza kazi waliyopewa ndani ya muda uliopangwa; c) Kudhibiti maadili ya wanafunzi;
d) Kuadhibu tabia mbaya ya wanafunzi na kuziondoa kabisa;
e) Kuhakikisha mwanafunzi anafikia kiwango cha alama 70 kwa kila somo;
f) Katika kutekeleza kanuni hizi, Mkuu wa Shule /Msaidizi wake atakuwa na mamlaka ya:-
a) Kuchunguza na /kumtafuta mwanafunzi na mali zake wakati wowote inapohitajika;
b) Kutumia nguvu zinazofaa na kumpa adhabu yoyote;
c) Kumchukulia mwanafunzi hatua zozote za kinidhamu awapo ndani ya eneo la Shule inapohitajika.

## 2.3. Kanuni za Shule.

i. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule na nje ya geti bila idhini ya maandishi kutoka kwa Mkuu wa Shule au Makamu wake ikibainika anafukuzwa shule;
ii. Kila mwanafunzi lazima avae sare ya shule anaposafiri kwenda nje ya shule na hata wakati wa kurudi kuja shuleni;
iii. Hairuhusiwi mwanafunzi kula nje ya bwalo la chakula;
iv. Mavazi, nyenzo na vifaa visivyoruhusiwa shuleni ni pamoja na :-
    i kisu; ii Silaha; iii Pombe; iv Dawa haramu; v Vitu vilivyoibwa; vi Tumbaku na sigara; vii Picha za ngono; viii Simu ya rununu, kompyuta ndogo, redio, kimemeshi (charge); ix Fataki; x Mavazi tofauti na yale yaliyoidhinishwa na uongozi wa shule; xi Vyakula kama- sukari, maziwa na peanut butter.
v. Kutembelewa kwa wanafunzi kutafanywa tu kwa wazazi/walezi walioidhinishwa au kuthibitishwa na uongozi wa shule na kwa kibali maalumu kutoka kwa mkuu wa Shule au Makamu mkuu wa shule; ukileta vufaa hauruhusiwi kuonana na mwanafunzi.
vi. Mawasiliano yote ya nje lazima yafanywe kupitia msemaji wa Shule ( Mkuu wa Shule au Makamu mkuu wa Shule); au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na mkuu wa shule;
vii. Mgeni yeyote haruhusiwi kuingia katika mabweni ya wanafunzi bila idhini kutoka kwa mamlaka husika;;
viii. Kiingereza ndio lugha rasmi itakayotumika shuleni. Wanafunzi wote lazima wawasiliane kwa lugha ya Kiingereza kipindi chote wawapo shuleni au wakienda kanisani na msikitini.

### 2.3.2: Usimamizi wa Programu zingine za Shule

i. Wanafunzi wote wanapaswa kuzingatia programu zote za kila siku za shule kwa ukamilifu. Kutohudhuria baadhï ya masomo / mitihani, kuchelewa, au kutohudhuria baadhi ya programu kutatolewa adhabu ya kufukuzwa shule;

ii. Wanafunzi wote wanapaswa kuzingatia usafi wa miili yao, nguo, usafi wa mabweni na mazingira muda wote;

iii. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie na kukamilisha kazi aliyopewa ndani ya muda uliowekwa na mamlaka husika kinyume chake atapewa adhabu kali.

**2.3.3: Mwenendo Kuhusiana na wanafunzi wenzao, Walimu na wafanyakazi pamoja na Utawala wa shule kwa ujumla.**

i. Kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia maelekezo/amri zote halali kutoka kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu kugoma kutii maelekezo kutasababisha kufukuzwa shule;.

ii. Kila mwanafunzi anapaswa kuishi na mwanafunzi mwenzake kwa heshima, uaminifu na ushirikiano;

iii. Uonevu kwa mwanafunzi/wanafunzi mwenzako, walimu au mwanajamii mwingine yeyote ndani ya shule ni kosa kwa mujibu wa taratibu za shule;

iv. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujihusisha na ndoa/mapenzi na hata mapenzi ya jinsia moja na kuchangia kitanda kulala au kukaa utafukuzwa shule;

v. Kugombana au kupigana na wanafunzi wenzako, walimu pamoja na mfanyakazi mwingine yeyote ni kosa la kufukuzwa shule mara moja;

vi. Wizi hauruhusiwi na atakayebainika atafukuzwa shule mara moja.

**2.3.4: Mwenendo kuhusiana na Mali za shule.**

i. Uharibifu wa mali za shule ni kosa linaloweza kusababisha kufukuzwa shule pia kugusa, kuchafua ukuta wa shule utawajibika kununua rangi na gharama zote utawajibika nazo.

**3.3.5: Adhabu kutokana na mwenendo mbaya**

i. Wanafunzi wote wenye mwenendo usioridhisha, utovu wa nidhamu, uvunjaji wa sheria za shule au kushindwa kufuata maelekezo yanayofaa yaliyotolewa na mwalimu au wafanyakazi wa shule watafukuzwa shule kwa kuzingatia sheria na taratibu za shule.

**3.3.6: Namna ya kurekebisha tabia mbaya ya mwanafunzi / tabia isiyoridhisha.**

i. Karipio Ia mdomo;

ii. Kazi ya ziada au kurudia kazi isiyoridhisha hadi ifikie kiwango kinachotakiwa;

iii. Kuripoti mara kwa mara ofisini kadiri itakavyoamuliwa;

iv. Kulipia mali za shule ulizoziharibu;

v. Adhabu ya viboko kwa kuzingatia mwongozo wa Serikali;

vi. Kusimamishwa masomo shuleni kwa muda (kwa muda wa siku 14);

vii. Kufukuzwa shule moja kwa moja;

viii. Kusimamishwa kwa muda kwa siku 14 na kugharamia mali uliyoiharibu.

**3.3.7: Masharti ya kutekeleza adhabu**

i. Adhabu zinapaswa kutekelezwa mara kwa mara na kwa usawa kulingana na sheria hizi;

ii. Adhabu zilizowekwa hazipaswi kamwe kuhatarisha usalama wa mwanafunzi. Walimu wanapaswa kuepuka kumweka mwanafunzi katika hatari kwa:-

a) Kukagua ikiwa mwanafunzi ana ugonjwa unaojulikana jambo ambalo litasababisha adhabu kuwa hatarishi kwa maisha ya mwanafunzi.

b) Kuangalia ikiwa mzazi anaweza kufahamishwa kuhusu tatizo Ia mwanafunzi.

iii. Adhabu inapaswa kulingana na uzito wa kosa lililotendwa pamoja na umri wa mwanafunzi.

### 2.3.8.Makosa na vikwazo

i. Ukiukaji wa kifungu cha 2.3-l(i); kuadhibiwa kupitia kifungu cha 2.3.6 (ix) na au (x) ii. Kifungu cha 2.1(i),(iv); kitatumika kifungu cha 2.3.6 (i), (iv).

iii. Kukiuka kifungu cha 2.1 (iv); kitatumika kifungu 2.3.6 (ix) na au 2.3.6 (viii).

iv. Kifungu cha 2,3 (i) hadi (iii) kuadhibiwa kupitia kifungu cha 2.3.6 (i) hadi (v)na au (x) ambapo kosa linahusisha mitihani iliyoratibiwa.

v. Kosa linalohusiana na kifungu cha 2.3.6 (i) hadi 2.3.2 (iii); litaadhibiwa kwa kuzingatia adhabu za kifungu cha 2.3-l(i) hadi(iv)

vi. Kutenda kosa linalohusiana na kifungu cha 2.3.2 (iv), (v) na (vi), kuadhibiwa kupitia 2.3.6 (viii) na (x).

vii. Kutenda kosa linalohusiana na kifungu cha 2.3.2 (vii) na 2.3.6 (i);kutaadhibiwa kulingana na adhabu ya kifungu cha 2.3.6 (viii) na au 2.3.6 (x).

viii. Utenda wa kosa linalohusiana na 2.3-1 (i), unaweza kuadhibiwa chini ya kifungu cha 2.3.6 (viii), (ix) na au (xi).

3. Shukrani:

Mimi ________________________________________Mzazi/MIezi wa kidato cha______ NATHIBITISHA kuwa nimepokea, kusoma na kuelewa kanuni; na sheria zote na ninaahidi kuzizingatia ipasavyo.

**Saini:______________________________ Tarehe:________________________________**

WHITE LAKE HIGH SCHOOL
P.O. Box 75787, Changanyikeni, Dar es Salaam, Tanzania.
Regn. No: S.1388
Tel: 0738 -783331 / 0738 -783332 / 0738 -783333
website: www.whitelakehighschool.co.tz / email: info@whitelakehighschool.co.tz

**WHITE LAKE HIGH SCHOOL APPLICANT STUDENTS MEDICAL EXAMINATION FORM**

## 3.1 Student's medical information:

***(To be filled in by authorized medical Doctor only)***

Doctor's name:____________________________ Residence ____________________ Telephone office __________________________ Mobile ____________________________

Hospital ________________________________Location _______________________________
Hospital Telephone Number _____________________________________________________

Please indicate if the student has the following problems and mark where appropriate,

1. Asthma. ☐ 2. Eye sight. ☐ 3. Hearing ☐

4. Wears glasses Medication. ☐ 6. Allergies ☐

Medical Allergies (Describe) ____________________________________________________

__________________________________________________________________________

What is his/her blood group? _____________________________________________________
Any serious illness? _____________________________________________________________
Any diagnosed learning disability? ________________________________________________

I acknowledge that the information provided above is accurate to the best of my knowledge and understanding.

Sign & Stamp ____________________________Date

_____________________________ (Doctor)

……………………………………….Official Use………………………………………

Verified by: ____________________________________________________

Remarks: _________________________________________________________________

Signature __________________________Date: ___________________________________

**4. 0 UTHIBITISHO:**

Mimi/Sisi (Taja jina la mzazi) ____________________________________ mzazi/mlezi/walezi wa mwanafunzi _____________________________, ninathibitisha kuwa taarifa zote zilizotolewa hapo juu ni sahihi kadiri tunavyofahamu na kwa hivyo nathibitisha kwa dhati kwamba, ikiwa mtoto wangu atakubaliwa katika Shule ya Sekondari White Lake; itashirikiana kwa karibu na uongozi wa shule kuchochea ukuzaji wa maadili na kielimu wa mtoto wangu. Ninaingia katika makubaliano na shule baada ya kusoma kwa makini na kuelewa maelekezo ya usajili na maagizo mengine yaliyoainishwa humu. Kwa hiyo:-

(i) Ninaahidi kulipa ADA ya Shule na mahitaji mengine yote ya Shule yanayohitajika shuleni kwa wakati uliowekwa ili kuwezesha taasisi kufanya kazi vizuri.

(ii) Ninaidhinisha shule kuchukua hatua kamili kwa mwanangu kwa lengo la kuboresha mwenendo wa mtoto wangu.

(iii) Nimesoma sheria za Shule na ninaahidi kumshauri mwanangu kuzingatia; vinginevyo nitazingatia uamuzi huo endapo mwanangu atakiuka kwa namna yoyote ile;

(iv) Ninaelewa na kukubali kwamba mwanangu LAZIMA afikie wastani wa alama 70 ili aweze kuendelea na darasa lingine; vinginevyo atalazimika kukariri darasa au atalazimika kuhama shule.

Sahihi ya Mzazi:

Tarehe ya kusaini:

**KWA MATUMIZI YA OFISINI TU:**

(i) Darasa lililokubaliwa:

(ii) Tarehe ya kujiunga:

(iii) Nambari ya kuingia:

(iv) Maoni ya Mkuu wa shule:

(v) Jina la Mkuu wa shule:

Saini

Tarehe

Tarehe &Muhuri

**4.1 TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI**

**A) TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI WA KIUME (BABA)**

i. Jina kamili [ ] [ ] [ ]
***JINA LA KWANZA*** ***JINA LA KATI*** ***JINA LA UKOO***

ii. Kitongoji [ ]

iii. Kijiji / Mtaa [ ]

iv. Kata [ ]

v. Wilaya [ ]

vi. Mkoa [ ]

vii. Utaifa [ ] Dini [ Dhahebu ] Dhehebu [ ]

viii. Sanduku la Posta [ ]

ix. Simu ya nyumbani [ ]

x. Kazi [ ]

**B) TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI WA KIKE (MAMA)**

i. Jina kamili [ ] [ ] [ ]
***JINA LA KWANZA*** ***JINA LA KATI*** ***JINA LA UKOO***

ii. Kitongoji [ ]

iii. Kijiji / Mtaa [ ]

iv. Kata [ ]

v. Wilaya [ ]

vi. Mkoa [ ]

vii. Utaifa [ ] Dini [ Dhahebu ] [ ]

viii. Sanduku la Posta [ ]

ix. Simu ya nyumbani [ ]

x. Kazi [ ]